

*Copyright from left to right © ICCROM - WCSM - NCAM; © World Monuments Fund; © World Monuments Fund; © Yoohoo Media*

# Kuunganisha Urithi wa Utamaduni

Ili kutuma ombi

## Ni nini?


***Kuunganisha Urithi wa Utamaduni*** ni programu ya kimataifa ya kujifunza baina ya wanarika kwa ushirikiano na watu wanaohusika katika kulinda urithi wa utamaduni. Kupitia mfululizo wa vikao vya mtandaoni kwa kipindi cha miezi 11, programu hii huleta pamoja watu 30 kujifunza na kusaidiana, ikilenga kile kinachofanya kazi (na kisichofanya kazi) katika Ulinzi wa Urithi wa Utamaduni.

Programu ya ***Kuunganisha Urithi wa Utamaduni*** imeundwa ili kuwezesha kila mtu kushiriki uzoefu wake: yale uliyojifunza, mazoezi yako, changamoto zako na mawazo mazuri. Lengo kuu ni kukusaidia katika kazi yako ya baadaye kwa kuongeza uhakika, maarifa na mitandao yako ya usaidizi.

### Muundo wa Programu

Programu ya ***Kuunganisha Urithi wa Utamaduni*** iliundwa kwa kushirikiana na wataalamu na mashirika mbalimbali wanaofanya kazi katika ulinzi wa urithi wa utamaduni kutoka Mashariki ya Kati, Afrika Kaskazini, Afrika Mashariki na Asia Kusini. Ina mizunguko mitatu ya wiki 8, kila moja ikiwa na mwelekeo tofauti unaohusiana na ulinzi wa urithi wa utamaduni:

1. Kwanza, tutachunguza mazoea yenu kama wataalamu katika ulinzi wa urithi wa utamaduni. Mada zinazowezekana: kuunga mkono mazoea ya kiasili na ya kitamaduni, kuleta maana, maendeleo endelevu na kushughulikia mabadiliko ya tabianchi.
2. Katika mzunguko wa pili, tutashughulikia changamoto mbalimbali za usimamizi.
   Mada zinazowezekana: tathmini na kujifunza, ufadhili, kufanya iwe ya kidijitali, kuhifadhi nyaraka na kuweka kumbukumbu na kusimamia uanuwai.
3. Katika mzunguko wa mwisho, tutafikiria kuhusu utetezi na kuitetea kazi yetu.
   Mada zinazowezekana: ushirikiano na miungano, mahusiano ya kitamaduni, kuzungumza na watunga sera na kutetea urithi wa utamaduni.



Katika kila mzunguko kutakuwa na kikao cha utangulizi, kikifuatiwa na vikao vya vikundi vidogo vya mada na tutamalizia kwa kikao cha muhtasari. Baada ya kila mzunguko, tutakuwa na wakati wa kutafakari kuhusu programu na kushiriki mafunzo. Kama mshiriki, utaweza kupendekeza na kuchagua masuala na mada kwa ajili ya uchunguzi katika kila mzunguko.

Julai 2023 – Mei 2024

Takribani saa 35 za vikao vya mtandaoni kwa jumla na baadhi ya kazi za nje ya mtandao

Vikao vya programu vitawasilishwa kupitia Zoom. Pia kutakuwa na chaneli ya mtandaoni ya kuwasiliana na washiriki wengine na timu ya utoaji wa programu.


Programu hii itaendeshwa kwa Kiingereza, hata hivyo usaidizi unapatikana kwa idadi ndogo ya lugha.

Utalipwa £1200 kwa kuhusika kwako, itakayolipwa kwa awamu mbili, ya kwanza mwanzoni mwa programu na ya pili baada ya kukamilika kwa programu.

## Ni kwa ajili ya nani?

Programu ya ***Kuunganisha Urithi wa Utamaduni*** imeundwa kwa ajili ya watu ambao:

- Wanahusika kikamilifu katika ulinzi wa urithi wa utamaduni.
- Wana jukumu kama vile kiongozi/mratibu wa jumuiya, mtaalamu wa urithi wa utamaduni, kiongozi wa mradi/meneja
- Wana uzoefu wa kufanya kazi katika ulinzi wa urithi wa utamaduni katika mojawapo ya nchi zinazostahiki:
    - **Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini**: Algeria, Misri, Iraki, Yordani, Lebanoni, Libya, Maeneo ya Palestina Yanayokaliwa kwa Mabavu, Syria, Tunisia, Yemeni
    - **Afrika Mashariki:** Ethiopia, Kenya, Sudan, Tanzania, Uganda
    - **Asia Kusini:** Bangladeshi, Nepali, Pakistani



- Wamejizatiti kushiriki na kujifunza 'Kinachofanya Kazi katika Ulinzi wa Urithi wa Utamaduni' na wenzao wa kimataifa
- Wanaweza kushiriki mtandaoni (upatikanaji wa intaneti na Zoom wakati wa vikao vya kikundi na majukwaa ya kushiriki taarifa kati ya vikao)
- Wana ujuzi fulani wa kufanya kazi kwa kuzungumza Kiingereza

Kushiriki katika programu ni kwa njia ya maombi. Washiriki watachaguliwa kwa msingi wa kufaa kwao kwa programu na kufikia usawa mzuri wa ujuzi, uzoefu na maslahi katika kikundi.

Tunatambua kwamba kuna gharama ya kushiriki katika maendeleo ya kitaalamu, kwa hivyo tunatoa "ada ndogo ya ushiriki" kwa washiriki wote ili kuunga mkono usawa wa ufikiaji.

### Matarajio

Ikiwa umechaguliwa kushiriki katika programu hii, tutatarajia:


- Ujizatiti kwenye programu hii na uwe sehemu amilifu ya kikundi.
- Uwe tayari kuzungumza kuhusu uzoefu wako mwenyewe wa ulinzi wa urithi wa utamaduni na kusikiliza uzoefu wa wengine.
- Uzingatie kanuni za kujifunza kwa kushirikiana, ikiwemo kuwa wazi, mwaminifu na kuheshimu juhudi na muktadha wa wenzako.
- Uwe mdadisi kuhusu kujifunza kwako na kuhusu kile unachoweza kujifunza kutoka kwa wengine.
- Ufikirie jinsi unavyoweza kushiriki mafunzo na matokeo na jumuiya yako au mashirika na mitandao mbalimbali kando na programu.
- Uwajibikie mafunzo yako mwenyewe. Tutakualika utambue eneo fulani la uchunguzi na ufuatilie hili wakati wa programu kupitia "logi ya kujifunza" au shajara ya mtu binafsi.
- Ushiriki katika vikao vyote vya kikundi kamili na angalau vikao vitatu vidogo vya kikundi wakati wa kila mzunguko.
- Utafakari na utoe maoni kuhusu yale uliyopitia katika programu nzima kwa madhumuni ya tathmini.

## Ninawezaje kutuma ombi?

[Ili kutuma ombi]

Ili kutuma ombi, [tafadhali jaza fomu hii ya maombi.]

Ikiwa unafaa wasifu wa mwombaji, ulioainishwa hapo juu tafadhali jibu maswali ya maombi kwa kutoa maelezo mengi kadiri uwezavyo ndani ya kikomo cha maneno ulichopewa. Si lazima utumie kikomo kamili



cha maneno au utupe maelezo mengi kuhusu miradi mahususi lakini ni muhimu utupe ufahamu mzuri wa mambo yanayokuvutia na uzoefu katika ulinzi wa urithi wa utamaduni.

## Kuwasilisha ombi lako

Mara baada ya ombi lako kukamilika, tafadhali hakikisha kwamba unabofya kitufe cha ‘Wasilisha’ ili utume ombi. Barua pepe itatumwa kwako ikithibitisha uwasilishaji wako.

Tafadhali hakikisha kwamba ombi lako limewasilishwa kabla ya tarehe ya mwisho ya 19 Juni 2023 saa tatu asubuhi (9:00) majira ya BST, kwani ombi lako halitazingatiwa ikiwa litawasilishwa baada ya tarehe ya mwisho.

## Mchakato wa Uteuzi


Kwa kutumia mchakato wa tathmini wenye uwazi, uteuzi wa mwisho wa washiriki wa programu utazingatia vigezo vifuatavyo:

- Jinsi unavyolingana na wasifu uliokusudiwa (angalia **ni kwa ajili ya nani** hapo juu)
- Nia yako ya kuungana na wengine na kuchangia ‘kile kinachofanya kazi’ kwa ulinzi wa urithi wa utamaduni
- Umuhimu wa maslahi na uzoefu wako kwenye programu na malengo yake
- Kufikia mchanganyiko mzuri wa ujuzi, maslahi na uzoefu wa kitaalamu (ikiwemo urefu na aina ya uzoefu, iwe umefanya kazi katika urithi ndani ya mazingira ya jumuiya au ndani ya shirika la urithi)
- Kufikia mchanganyiko wa uzoefu wa maisha, jinsia na kuenea kwa kijiografia katika nchi zinazostahiki

Programu hii itaendeshwa kwa Kiingereza, hata hivyo tutaweza kutoa nyenzo zilizotafsiriwa na kutoa usaidizi wa ukalimani wakati wa vikao kwa idadi ndogo ya lugha.

Maombi yataorodheshwa kulingana na vigezo vya uteuzi kama ilivyo hapo juu. Maamuzi ya mwisho yatafanywa na jopo, kwa kuzingatia vipengele kama vile usawa wa ujuzi, uzoefu na maslahi katika ulinzi wa urithi wa utamaduni.

Utatumiwa barua pepe kuhusu matokeo ya maombi yako ifikapo tarehe 26 Juni 2023. Ukichaguliwa, utaombwa kutia saini Mkataba wa Mafunzo ambao unaelezea jukumu lako, wajibu na kujizatiti kwako kwenye programu.



## Maswali na Taarifa Zaidi


Ikiwa una maswali yoyote kuhusu programu au mchakato wa maombi, tafadhali tuma barua pepe kwenda caitlin.wagner@theaudienceagency.org.

Ikiwa ungependa kujua zaidi kuhusu programu na kuzungumza na mmoja wa washirika wetu katika eneo lako, tafadhali tuma barua pepe kwa mshirika husika:

- Mashariki ya Kati na Afrika Kaskazini: Al-Mawred Al-Thaqafy
- Afrika Mashariki: Bayimba Foundation
- Asia Kusini: Asia-Europe Foundation

Tutafanya kikao kifupi cha kutoa maelezo kuhusu programu tarehe 8 Juni saa tatu asubuhi (9am) majira ya BST ambapo tutaweza pia kujibu maswali yoyote ambayo unaweza kuwa nayo. Kikao cha kutoa maelezo kitafanyika kwa Kiingereza. Kuhudhuria ni hiari na maelezo kutoka kwenye kikao hicho yatashirikiwa kwenye ukurasa huu kufuatia tukio hilo. Tafadhali jisajili kuhudhuria na upokee kiungo kwa ajili ya kikao hicho hapa.

Ili kutuma ombi



# Kutuhusu

Programu ya *Kuunganisha Urithi wa Utamaduni* inatolewa na [The Audience Agency](), [Bayimba](), [Asia-Europe Foundation]() na [Culture Resource]()kama sehemu ya programu ya Kile Kinachofanya Kazi ya Mfuko wa Ulinzi wa Utamaduni wa British Council.

Programu ya *Kuunganisha Urithi wa Utamaduni* iliagizwa na [British Council]() kama sehemu ya kazi ya Mfuko wa Ulinzi wa Utamaduni ili kusaidia kukuza uhakika, maarifa na mitandao ya wataalamu. Programu hii pia itasaidia kufahamisha mafunzo na mazoezi bora kwa mbinu ya British Council ya kujifunza baina ya wanarika na kwa ushirikiano.

Mfuko wa Ulinzi wa Utamaduni (CPF) unaongozwa na British Council kwa kushirikiana na Idara ya Serikali ya Uingereza ya Kidijitali, Utamaduni, Vyombo vya Habari na Michezo (DCMS). Lengo kuu la mfuko huu ni kusaidia kuunda fursa endelevu za maendeleo ya kijamii na kiuchumi kupitia kujenga uwezo wa kukuza, kulinda na kuendeleza urithi wa utamaduni. CPF inatoa ufadhili kwa miradi inayoweka maeneo ya urithi wa utamaduni na vitu salama, pamoja na kusaidia kurekodi, kuhifadhi na kurejesha urithi wa utamaduni. Pia hutoa fursa kwa jumuiya za maeneo husika kwa mafunzo na elimu, kuwawezesha kwa muda mrefu kuthamini, kutunza na kufaidika na urithi wao wa utamaduni. Tangu mwaka 2016 Mfuko wa Ulinzi wa Utamaduni umetoa zaidi ya £ milioni 35 kwa miradi 112 katika nchi 16.

Programu ya *Kuunganisha Urithi wa Utamaduni* ni sehemu ya Programu ya Mfuko wa Ulinzi wa Utamaduni ya 'Kinachofanya Kazi', inayolenga kusaidia matokeo bora zaidi ya ulinzi wa urithi wa utamaduni na jumuiya za maeneo husika kwa kuleta ushahidi bora unaopatikana kwa wataalamu na wafanya maamuzi wengine katika sekta ya kimataifa ya ulinzi wa urithi. Kwa kushiriki utafiti wenye taarifa, mbinu za kufanya maamuzi, mbinu bora zaidi na mafunzo waliyojifunza, inalenga kukuza ushirikiano zaidi, kuchangia matokeo yaliyoratibiwa zaidi katika sekta zote za ulinzi na maendeleo ya urithi wa utamaduni. Mbinu ya Kinachofanya Kazi inazingatia ufikiaji bora wa ushahidi wa hali ya juu unaoweza kutumika katika ulinzi wa urithi wa utamaduni; kuongezeka kwa motisha ya kutumia ushahidi; kuboreshwa kwa uwezo wa kutumia ushahidi vizuri na kuongezeka kwa fursa za kutumia ushahidi katika kufanya maamuzi.

Pata maelezo zaidi kuhusu washirika kwa kubofya nembo zilizo hapa chini: